OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA.

MKOA WA KILIMANJARO NYERERE SHULE YA SEKONDARI

Simu Na. 0782 333 663 / 0754 818 362 S.L.P 233

KUMB NA NYSS/GEN/VOL.IV/JOINING INSTR. FV **MWANGA**

…….

ANUANI: ……..

YAH: FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYERERE KIDATO CHA TANO MWAKA 2018/19

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga Kidato cha Tano katika shule hii. Jumuiya ya Shule ya Sekondari Nyerere (Mwanga) inasema KARIBU na HONGERA SANA KWA KUCHAGULIWA. Ni mategemeo yetu utafurahia maisha ya Shule kwa muda wote utakapokuwa ukisoma hapa na kwamba utaonyesha tabia njema, ari ya kujifunza na kutekeleza shughuli zote zinazomhusu mwanafunzi kwa bidii na maarifa.

Shule iko Mkoani **Kilimanjaro**, Wilaya ya Mwanga, Kijiji cha Lembeni kilometa 15 kutoka Mwanga mjini kuelekea Same. Au kilometa 40 kutoka Same kuelekea Mwanga. Shule iko karibu na barabara kuu ya kutoka **Dar es salaam** kwenda **Arusha** takribani mita 500.

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe …… kuanzia saa 8.00 mchana. Endapo utachelewa kuripoti bila kutoa taarifa baada ya mwezi mmoja kupita utakuwa umepoteza nafasi hii. Utapokelewa ukiwa na mahitaji yafuatayo;-

A. MAHITAJI YA SHULE:

S/N	AINA YA MAHITAJI	MUHULA I	MUHULA II
1.	Ada	35,000/=	35,000/=
2.	Mchango wa Ukarabati	15,000/=	
3.	Mchango wa Taaluma	10,000/=	10,000/=
4.	Mchango wa walinzi, wapishi na vibarua wengine	15,000/=	15,000/=
5.	Mock	20,000/=	
6.	Kitambulisho	6,000/=	
7.	Tahadhari (Haitarejeshwa)	5,000/=	
8.	Godoro	10,000/=	10,000/=
9.	Nembo	2,000/=	
10.	Bima ya Afya	5,000/=	

11	Huduma ya kwanza	5,000/=	
	Jumla ya michango	**128,000/=**	**70,000/=**

Malipo haya yote yalipwe kwenye Akaunti ya shule. Akaunti Na. 40201100006 – Lembeni Secondary School. Benki ya NMB Mwanga. Kisha utuletee Bank Pay in Slip (BPS) ikiwa inaonyesha majina kamili na mchepuo wa mwanafunzi. Fedha taslimu haitapokelewa hapa shuleni.

B. **MAHITAJI YA DARASANI**:

I. Madaftari makubwa ya masomo 5 (counter book)

II. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa sayansi

III. Rimu ya karatasi A4 anapaswa kuikabidhi kwa kila mwaka.

IV. Baadhi ya vitabu kulingana na masomo yake.

V. Mathematical set 1

VI. Graph pad

C. SARE ZA SHULE NA MAHITAJI MENGINE MUHIMU:

- Shati mbili nyeupe mikono mifupi na moja uje akiwa amelivaa.
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba (gidamu)
- Socks za rangi yoyote
- Mkanda mweusi wa ngozi usio na baikrosi kubwa
- Sweta litapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 16,000/=
- Jezi (bukta na Tshirt) rangi ya blue, viatu vya michezo.
- T shirt yenye nembo ya shule itapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 8,000/=
- Suruali mbili zitashonwa shuleni kwa gharama ya sh. 20,000/= kila moja.
- Suruari mbili nyeusi za kitambaa moja aje ameivaa.
- Shuka mbili za bluu bahari (Light blue) na chandarua
- Sanduku linalofunga vizuri la chuma.

ZINGATIA: Nguo ambazo sio sare ya shule haziruhusiwi kabisa. Ukaguzi utafanyika mara baada ya kuwasili shuleni.

D. VIFAA VYA USAFI SHULENI:

- ✓ Ndoo ndogo mbili za lita 10 moja utakabidhi nyingine ya matumizi yako binafsi.
- ✓ Sahani, kikombe, bakuli, kijiko.

- ✓ Brush ndogo za kusugulia sink.
- ✓ Ufagio chelewa
- ✓ PCB na CBG aje na Jembe na mpini wake.
- ✓ HGK aje na Reki na Panga.
- ✓ Hard broom/soft broom/mopa.

E. MAELEKEZO:

Fomu zifuatazo zijazwe na uje nazo shuleni zikiwa kamili:-

1. Fomu ya kukubali masharti
2. Sheria na taratibu za shule.
3. Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi na mzazi
4. Nakala ya cheti cha kuzaliwa uje nacho
5. Nakala ya Result slip ya kidato cha nne uje nayo
6. Medical Examination form

Kwa kumalizia nakutakia maandalizi mema na safari njema kuja kujiunga katika shule hii. Utakapofika daima kumbuka kuwa msimamo wa shule hii ni kuzingatia ELIMU, JUHUDI, KAZI NA MAARIFA.

MOTTO WA SHULE NI "BUILD FOR THE FUTURE GENERATION"

KARIBU SANA NYERERE SEKONDARI



R.M. KAGUSHA

MKUU WA SHULE

HEADMASTER
NYERERE SECONDARY **SCHOOL**
MWANGA-KILIMANJARO

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha, wanafunzi wote wanatakiwa kuzingatia haya yafuatayo:

Kila mwanafunzi anayejiunga na shule hii anapaswa kutambua kuwa yupo hapa kwa ajili ya **KUSOMA** kwa faida yake, familia yake na Taifa lake kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, chochote kilichopo nje ya jukumu hili hakina nafasi katika shule hii.

Mahudhurio;

- Kuwahi shuleni ni wajibu wa kila mwanafunzi, hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni tarehe ya kufungua shule bila kukosa na kuendelea kuwepo shuleni kila siku.
- Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na nje ya darasa. Vipindi vya kazi za mikono pamoja na michezo ni sehemu ya masomo.
- Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria mikusanyiko halali yote ya shule kama vile, mstarini, usafi, Baraza la shule, Ibada, midahalo (Debates), n.k.
- Ni lazima kutimiza kwa makini mahudhurio ya maandalio ya jioni (Evening Preparation).
- Kila mwanafunzi anawajibika kuwahi kula chakula kwa wakati uliopangwa. Ni marufuku kuwahi kuchukua chakula kabla ya wengine wote. Kama kuna tatizo lolote liripotiwe kwa mwalimu wa zamu / wa chakula kwanza.

Sare za Shule.

- ✓ Wanafunzi wote ni lazima kuvaa sare ya shule muda wote wa darasani na wanapotoka nje ya shule.
- ✓ Mwanafunzi lazima ajiweke katika hali ya usafi kimwili na kimavazi. Nguo zote atakazovaa mwanafunzi lazima zikubaliwe na uongozi wa shule pale anaporipoti mwanafunzi shuleni tu.
- ✓ Nguo za michezo huvaliwa wakati wa michezo tu.

Heshima na Utii.

- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema popote alipo ndani na nje ya mipaka ya shule.
- Kila mwanafunzi anatakiwa kutii kengele, kutii na kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wote, Viranja wa shule na Jumuiya nzima ya shule.
- Mwanafunzi anatakiwa kusimama /kumpokea na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita au aingiapo shuleni au darasani.
- Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, fedha za Taifa, Wimbo wa Taifa, Wimbo wa Shule, Nembo ya Taifa na Picha za viongozi wa Serikali.
- Kiranja yeyote wa shule anatakiwa kula kiapo cha utii na kuwa mfano katika kutekeleza kanuni na taratibu za shule. Kukiuka taratibu za shule kunaweza kumpotezea sifa ya kuwa kiongozi na adhabu nyingine kuchukuliwa dhidi yake ikiwa pamoja na kusimamishwa / kufukuzwa shule. Mkuu wa shule ana mamlaka ya kuteua kiongozi mwingine wakati wowote pale itakapobidi.

Sehemu muhimu za Kujifunzia:

a. Madarasa, Maabara na Maktaba ni sehemu za masomo, hivyo ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele, kuzomea, kupiga gumzo au kuzurura ndani ya sehemu hizo. Hairuhusiwi kutumia viti na madawati kusomea nje ya madarasa. Ikithibitika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.
b. Ni marufuku kuingia kwenye Maabara bila ya kibali cha mwalimu husika.
c. Ni lazima kila mwanafunzi atumie Maktaba kufuatana na sheria za maktaba.

Afya:

Kila mwanafunzi lazima ajiweke katika hali nzuri ya kiafya ili aweze kuyamudu masomo yake vyema.

(i) Endapo mwanafunzi ataugua ataomba ruhusa kwa mwalimu wa zamu/ mwalimu mshauri wa wanafunzi kama ataenda hospitali na kurudi siku hiyohiyo. Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na Mkuu wa Shule tu.
(ii) Gharama za matibabu zilizonje ya bima zitagharimiwa na mzazi/mlezi wako.
(iii) Mwanafunzi hatakiwi kuchafua mazingira ya shule kwa namna yoyote ile mfano kutupa taka ovyo, kwenda haja kubwa na ndogo mahali pasipostahili n.k
(iv) .Mwanafunzi anapaswa kutunza mwili wake ikiwa ni pamoja na kukata kucha, kunyoa nywele na ndevu, kutandika kitanda, kuoga, kupiga mswaki, na kupanga vitu vizuri bwenini n.k.

Mipaka ya Shule.

- Mwanafunzi yeyote atakae toka nje ya mipaka ya shule lazima apate kibali cha Mwalimu wa zamu na awe amevaa sare ya shule.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo: vilabu vya pombe, Majumba ya starehe na Nyumba za kufikia wageni.

Vifaa na Mali ya Shule.

- Majengo ya shule, Samani, Vifaa vya kazi na vifaa vya masomo ni mali inayogharimu fedha nyingi sana, hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kuvitunza vizuri ili viweze kudumu kwa manufaa ya baadaye.
- Ni marufuku kuandika au kuweka alama /chata katika kuta, milango, madirisha, meza au dawati au kiti na vitu vingine ambavyo ni mali ya shule.
- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutoa taarifa kwa kiongozi /mwalimu mara tu uharibifu/kuvunja kifaa chochote cha shule unapotokea.
- Uharibifu wowote au upotevu wa kitu chochote cha shule lazima ufidiwe badala yake.
- Mali zote za shule utakazokabidhiwa utalazimika kuzirudisha zikiwa katika hali nzuri, vinginevyo utalipia uharibifu.

MAKOSA AMBAYO YANAWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI.

(i) Kumiliki au kukutwa na simu ya Mkononi. Ikikamatwa kwanza haitarudishwa kabisa kwa sababu yoyote ile na pia hatua nyingine kuchukuliwa kama vile kusimamishwa/kufukuzwa shule.
(ii) Wizi.
(iii) Uasherati/ubakaji /Ushoga au vyote kwa pamoja.
(iv) Ulevi wa aina yoyote au uvutaji wa sigara, bangi na madawa ya kulevya.
(v) Kupiga au Kupigana.
(vi) Kugoma (mfano kutokula chakula cha shule), Kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
(vii) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule/umma.
(viii) Kumpa mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya Shule.
(ix) Kuoa au kuolewa.
(x) Kudharau Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, Fedha za Taifa, Wimbo wa Taifa au Picha za Viongozi wa Serikali.
(xi) Utoro wa Shule, mahudhurio mabovu darasani au kukosa kufanya mitihani/majaribio/mazoezi bila taarifa au kibali maalum cha Mkuu wa Shule.
(xii) Kufanya makosa mengine ya jinai au uhaini kama vile kumiliki Baruti, Silaha za moto na mfano wa hayo.
(xiii) Kukataa adhabu ya mwalimu, kugomea au kumtukana mwalimu au mtu yeyote.
(xiv) Kuchelewa kufika shule, au kukosa kuwepo shuleni kwa siku 90 mfululizo bila taarifa rasmi.

FOMU YA KUKUBALI MASHARTI NA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.

Anwani yako: ..... ……..

S.L.P ……

Mkuu wa Shule,
NyerereSekondari,
S.L.P 233,
MWANGA.

Mimi ……..
(Majina rasmi kwa herufi kubwa kama yanavyoonekana kwenye vyeti) nimesoma na kuelewa vizuri maagizo na masharti ya kujiunga na kidato cha Tano hadi cha Sita mwaka 2018/19 hadi 2019/20 .

Ninaahidi kuwa nitayatimiza yote yaliyoandikwa pamoja na kanuni na taratibu nyingine nitakazopewa nifikapo/niwapo shuleni.

Ninaomba nipokelewe shuleni, na iwapo nitakwenda kinyume cha masharti, kanuni na taratibu hizo, nitakuwa tayari kupokea adhabu nitakazopewa kulingana na makosa nitakayokuwa nimeyatenda.

SAINI YANGU .....

TAREHE .....

ZINGATIA: **SEHEMU YA CHINI IJAZWE NA MZAZI/MLEZI.**

Mimi Mzazi/Mlezi..... .
Nimesoma kwa makini maelezo na kanuni, sheria na taratibu zote za Shule.

*Nipo/*sipo tayari kushirikiana na Shule wakati wote wa masomo kuhusu malezi ya kijana wangu.

SAINI YA ZAZI/MLEZI ..... TAREHE ..... .

ANUANI .....SIMU ..... E-MAIL ……..

Taarifa zake za maendeleo zitumwe kwa ……
S.L.P ……Simu ya mkononi: ……..

Endapo kuna Dharura aarifiwe ndugu wa karibu aitwaye: ……

Ambaye ni (uhusiano) …… Simu ya Mkononi: ……..

(i) Ikumbukwe kwamba wakati wa likizo wanafunzi wanasafiri kurudi kwa wazazi au walezi na si vinginevyo.

(ii) Kama kuna sababu yoyote itakayokuzuia kujiunga na shule hii, tunaomba usijaze fomu hii isipokuwa jina lako tu uitume fomu hii kwetu. Ni kitendo cha kiungwana kutoa taarifa.

(iii) Aje na Picha (4) za wazazi au walezi wa mwanafunzi wanaoweza kuja kumtembelea au kwa wito na namba zao za simu.

PRESIDENT'S OFFICE – RALG

MWANGA DISTRICT COUNCIL

NYERERE SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 233

MWANGA.

REF:NO.NYSS.33/JI/VOL.I/46

MEDICAL OFFICER INCHARGE (HOSPITAL/HEALTH CENTER)

…….

…….....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please examine Mr/Ms …… as his/her physical and mental fitness for admission as Form I students at Nyerere Secondary School in the year 2017.

Yours faithfully,



HEADMASTER
NYERERE SECONDARY **SCHOOL**
MWANGA-KILIMANJARO

I have examined Mr/Ms ……. As shown and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full-time secondary education in the following aspects:-

1. Vision with/without glasses: Right eye …… Left eye ……
2. Hearing: ……...……
3. Blood Pressure ……..…….. Hemoglobin ……
4. Urine (a) Albumen …….. (b) …….
5. Diseases: (a) Venereal diseases …… (b) Bilharzia ……
6. Pregnancy ……
7. Neurosis ……..
8. Is there any abnormality of: (a) The Heart …… (b) Lungs ……
9. Are there serious diseases like Tuberculosis ……, Epilepsy ……. Asthma ……. Diabetes …….. etc.

Signature of the Medical Officer: …… Date: ……

Station: ……. Designation: ……...